Mungu Aliye Mkuu Akifunuliwa Mbele Zetu

Nina Maandiko machache yaliyoandikwa ambayo ningetaka kunena nanyi kwayo, na natumaini ya kwamba Mungu atazibariki juhudi zetu dhaifu. Sasa, watu wengi wameshangaa kwa nini sisi ni watu wa kipekee sana na wenye makelele sana. Mnajua, hii ni aina tofauti ya—ya mkutano kuliko ile watu wa—wamezoea kuona; na kwa kawaida kila kitu huwa tayari kimepangwa mbeleni. Bali tunapohudhuria mikutano hii (ambayo nimetunukiwa sasa kwa miaka tangu ilipoanzishwa), ikiwa hatujui kile tutafanya, tunakuja na kujitolea wenyewe. Hilo ndilo jambo tu tunalojua kutenda, naye Mungu hufanya yaliyobakia. Kwa hivyo hiyo inatufanya watu wa kipekee sana.

2 Hivi majuzi mtu fulani alisema, "Wajua, ninyi watu ni—ni watu wa kipekee sana."

Nami nikasema, "vema, na—nakisia ndivyo tulivyo."

3 Nami nakumbuka mmoja wa ile mikutano. Ndugu Toy alikuwa akiniambia wakati mmoja juu ya maskini Mjerumani mmoja aliyesema kwamba alikuwa tayari ameupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na siku iliyofuata dukani, alimokuwa akifanya kazi, yeye angeinua mikono yake, na kumsifu Bwana, na kunena kwa lugha, na kuendelea tu sana. Na hatimaye, bosi wake akaja na kusema, "Heinie, una nini?"

4 Akasema, "Lo, niliokolewa." Yeye akasema, "Moyo wangu unabubujika tu kwa furaha."

5 Yeye akasema, "Vema, bila shaka umekuwa kule chini na kundi lile la wale nati kule chini."

6 Yeye akasema, "Naam! Mungu atukuzwe!" kasema, "Bwana ashukuriwe kwa ajili ya hizo nati." Akasema—akasema, "Chukua motokaa inayokuja barabarani." Kasema, "Itoe nati zote, huna kitu ila kundi la takataka. Na hiyo tu ni—ni karibu kweli, mwajua."

7 Siku moja huko California, nilikuwa nikitembea kwenye Barabara za Los Angeles, na nikaona mtu fulani aliyekuwa na maandishi kifuani mwake humu; nayo yalisema, "Mimi ni mpumbavu wa Kristo." Na kila mtu alikuwa akimtazama na nikaona wao wakigeuka na kumtazama baada ya kupita. Nami nikaona yafaa nifanye kama wengine. Na kwenye upande—mgongo wake alisema, "Je, wewe ni mpumbavu wa nani?" Nakisia sisi sote ni wa kuchekesha sisi kwa sisi, mwajua. Bali, wajua, ulimwengu hufuata utaratibu fulani sana hata jambo

fulani tofauti huonekana la kizembe sana, hata watu wakafikiria ya kwamba—kuna kasoro fulani. Kwa kawaida inamlazimu Mungu kufanya jambo lisilo la kawaida sana apate kuwarudisha watu kwenye Biblia tena.

8 Naweza kuwazia ya kwamba Nuhu alikuwa kama na—nati kwa wakati huo wa kisayansi alimoishi, kwa sababu wao walikuwa na—wangethibitisha hapakuwepo maji kule angani. Bali Mungu alisema yangekuweko mle, kwa hivyo Nuhu alipohubiri na kuamini hayo, akawa nati. Nami nawaazia kwamba Musa aliposhuka kwenda Misri, yeye alikuwa na—nati kwa Farao; bali kumbukeni, Farao alikuwa nati kwake pia. Kwa hivyo wao . . . Tunatambua hayo.

9 Hata Yesu alidhaniwa kuwa mzushi. Hiyo ni kweli. Martin Luther alikuwa nati kwa kanisa Katoliki, na John Wesley alikuwa nati kwa Angalikana. Kwa hivyo mwajua, wakati umekaribia sana wa nati nyingine; sivyo? Bali kabla yakuwa na nati, mwajua, ilibidi kuwe na skrubu kwanza kuifungilia. Kwa hivyo mwajua, Nuhu akiwa nati, yeye . . . Chukua nati; inavuta skrubu—huvuta kitu pamoja na kushikamanisha kitu. Kwa hivyo Nuhu aliweza kuwavuta wote walioamini akawaingiza safinani kuwatoa hukumuni kwa kuwa nati.

10 Twaona ya kwamba Musa aliwavuta Kanisa kutoka Misri kwa kuwa nati. Hiyo ni kweli. Nafikiri tunahitaji nati sasa kumvuta Bibi—Arusi kutoka kanisani. Tunahitaji kitu fulani sasa, nati nyingine.

11 Kwa hivyo sisi ni watu wa kipekee sana. Nami nilifikiri usiku wa leo, Mungu akipenda, ningejaribu kusoma Maandiko kuhusu hili, na ningenena nanyi kwa dakika chache tu, na kujaribu kuwaonyesheni kwa nini sisi ni watu wa kipekee hivyo.

12 Hebu na tufungue Maandiko sasa katika Wafilipi sura ya 2 na mlango 1 hadi 8, na II Wakorintho 3:6; na hebu tukasome kwa maana tunaamini, Neno la Mungu. Na sasa, kabla tu hatujasoma, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi.

13 Baba wetu wa mbinguni mwenye rehema, bila shaka sisi ni watu walioheshimiwa usiku huu kuishi katika wakati huu, na kuona mambo tunayoona yakiendelea, na kujua ya kwamba wakati umekaribia sana ambapo Yesu atakuja kwa ajili ya Kanisa Lake. Lo, hilo linasisimua mioyo yetu, Bwana.

14 Na tunapofungua kurasa hizi usiku wa leo, tunaomba ya kwamba utatupa somo kutoka kwa hili fungu; na Roho Mtakatifu afunulie mioyo yetu mambo yanayofaa na yanayompendeza Mungu. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

15 Mwajua, naamini nitawaulizeni kufanya jambo fulani. Ma—mara kwa mara mimi huuliza mambo mageni, nami natumaini siwaulizi cho chote kigeni sana. Bali tunapoahidi kuitii bendera, sisi sote husimama; na—na bendera inapopita, tunasimama—

ambayo inatupasa; kufanya hivyo; nasi hupiga saluti. Na tusimameni kwa miguu yetu tunapolisoma Neno, mkitaka. II Wakorintho 3:6.

Naye. . .ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya; si wa andiko, bali wa roho; kwa maana andiko huuwa, bali roho huhuisha.

Basi, ikiwa—basi, ikiwa huduma ya mauti iliyoandikwa na kuchorwa katika mawe, ilikuja katika utukufu, hata Waisraeli hawakuweza kuukazia macho uso wa Musa, kwa sababu ya utukufu wa uso wake; nao ni utukufu uliokuwa ukibadilika;

Je! huduma ya roho haitazidi kuwa katika utukufu?

Kwa maana ikiwa huduma adhabu ina utukufu, siuze huduma ya haki ina utukufu unaozidi.

Maana hata ile iliyotukuzwa haikuwa na utukufu hivi, kwa sababu ya utukufu uzidio sana. Kwa maana, ikiwa ile inayobatilika ilikuwa na utukufu, jinsi ama—zaidi sana ile ikaayo ina utukufu.

Basi kwa kuwa tuna taraja la namna hii, twatumia ujasiri mwingi;

Nasi si kama Musa alivyotia utaji juu ya uso wake, ili kwamba Waisraeli wasitazama sana mwisho wa ile iliyokuwa ikibatilika;

Ila fikira zao zilitiwa uzito. Kwa maana hata leo hivi, wakati lisomwapo Agano la Kale, utaji uo huo wakaa; yaani, haikufunuliwa kwamba huondolewa katika Kristo;

Ila hata leo; torati ya Musa isomwapo, utaji huikalia mioyo yao.

Lakini wakati wo wote watakapomgeukia Bwana, ule utaji huondolewa.

Si. . .*Basi "Bwana" ndiye huyo Roho; Walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru.*

Lakini sisi sote, kwa nyuso *usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo* kubadilishwa *tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.*

16 Na katika Wafilipi 2, tunasoma haya (kuanzia kifungu cha kwanza na kusoma hadi kifungu cha 8):

Basi ikiwako faraja yo yote katika Kristo, yakiwako matulizo yo yote ya mapenzi,. . .ushirika wo wote wa Roho, ikiwako huruma yo yote na rehema,

Ijalizeni furaha yangu, ili mwe na nia moja, wenye mapenzi mamoja, wenye roho moja, mki. . .mkinia mamoja.

Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno, bali kwa unyenyekevu, kila mtu amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake.

Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie. . .?. . .mambo ya wengine.

Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwemo pia ndani ya Kristo Yesu;

Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho;

Bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa mwanadamu;

Tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.

17 Na tuombe. Baba wa mbinguni, Neno hili kuu ambalo limesomwa usiku wa leo kutoka kwa Maandiko Yako Matakatifu, lifanye dhahiri sana mioyoni mwetu, hata tutaondoka hapa kama hao waliotoka Emau wakisema, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani," kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. (Mwaweza kuketi.)

18 Sasa, hili ni fungu la kipekee sana, bali nafikiri linafaa sana kwa wakati huu. Nataka kuzungumza juu ya somo la: *Mungu Aliye Mkuu Akifunuliwa Mbele Zetu.*

19 Sasa, tangu mwanadamu aweko, pamekuweko na shauku kuu katika moyo wa mwanadamu kujua alikotoka, na sababu ya kuweko kwake hapa, na anakoenda. Kuna Mmoja tu anayeweza kujibu hilo; huyo ni Yeye Yule aliyemleta hapa. Na mwanadamu daima ametaka kumwona Mungu.

20 Kule nyuma katika Agano la Kale tunaona ya kwamba Mungu alijificha Mwenyewe toka kwa wasioamini. Mungu yuna njia ya kipekee sana ya kuwashughulikia watu. Yeye hujificha toka kwa asiyeamini na kujifunua kwa anayeamini. Mungu hufanya hivyo. Yesu alimshukuru Mungu kwamba mambo haya aliwaficha wenye hekima na akili, akawafunulia watoto wachanga ambao wangejifunza. Kwa hivyo tunaona kwamba Mungu habadiliki katika tabia Zake, na Yeye daima anafanya kazi yake vivyo hivyo. Tunaona katika Malaki 3, ya kwamba Yeye alisema, "Mimi ni Mungu, sina kigeugeu." Kwa hivyo Yeye hutenda katika kanuni zile zile kila wakati.

21 Sasa, tuchukue kimoja cha Vitabu vya kale sana vya Biblia. Ayubu, mmoja wa watu wenye haki sana katika

siku zake, mtu mkamilifu katika sheria za Mungu—mtumishi, mungwana, mtumishi mwenye heshima—hata Mungu akasema, "Hapana mmoja aliye kama yeye duniani . . ." Lakini shauku yake wakati mmoja, ni kumwona Mungu . . . Yeye alijua ya kwamba kulikuweko Mungu, naye akajisikia kwamba angetaka kumwona Yeye, au kwa njia nyingine aende nyumbani Kwake na kugonga mlango, na kusema, "Ningetaka kuzungumza Nawe," aketi chini, azumgumze Naye, jinsi tungalifanya sisi kwa sisi. Tuna ufahamu. Hiyo ndiyo sababu tuko katika mikutano hii, ambapo tunakutanika na—na kunena mawazo yetu; na—na tunafahamiana sisi kwa sisi vizuri zaidi tunapozungumzana. Na wahudumu hufanya hivyo. Watu wa tabaka mbali mbali hufanya hivyo, huzungumzana mambo.

22 Na Ayubu . . . Mungu alikuwa halisi sana kwake, yeye alitaka kuona kana kwamba hangalienda na kupiga hodi mlangoni Mwake na—na kuwa na—kuhojiana Naye. Bali twaona ya kwamba Mungu kweli alinena Naye, bali alikuwa amejitia utaji. Alikuwa amejificha katika umbo la upepo wa kisulisuli. Naye akamwambia Ayubu ajifunge viuno; alikuwa atanena naye kama mtu. Ndipo akashuka katika upepo wa kisulisuli na—na kunena na Ayubu. Naye alijulikana kwa Ayubu kwa upepo wa kisulisuli, walakini hakumwona kabisa. Yeye angesikia tu upepo ukivuma na ukizunguka-zunguka mitini; na Sauti ikatoka kwenye huo upepo wa kisulisuli, bali Mungu alikuwa amefichwa katika huo upepo wa kisulisuli.

23 Tunaona kule chini Afrika (Afrika Kusini) wao hutumia neno *Amoyah*, ambalo maana yake ni, "Uweza usioonekana." Na uweza huu usionekana katika upepo wa kisulisuli ulikuwa na sauti iliyosikika. Ilimzungumzia Ayubu, walakini hakuona sura Yake kamwe, bali alifichwa kwake kwa upepo wa kisulisuli. Tunaona mmoja wa manabii wakuu wa Biblia, Musa, wa Agano la Kale, mmoja wa watumishi wa Mungu aliyechaguliwa, akateuliwa, mtumishi aliyekusudiwa tangu asili, yeye pia alitaka kumwona Mungu. Yeye alikuwa karibu sana Naye na aliishaona mambo mengi sana ya mkono Wake mkuu wa ajabu ukimwongoza na ukifanya mambo ambayo ni Mungu tu angaliyatenda. Yeye alitaka kumwona siku moja, naye Mungu akamwambia, "Nenda kasimame juu ya mwamba."

24 Na alipokuwa amesimama juu ya mwamba, Musa akamwona akipita. Aliona mgongo Wake. Naye alisema, "Ulionekana kama wa mtu," mgongo wa mtu. Walakini hakumwona Mungu, yeye aliona tu utaji wa Mungu.

25 Biblia ilisema, "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote, Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyo ndiye aliyemfunua." Kwa hivyo Musa alimwona amejificha kama mtu.

26 Nasi twaona ya kwamba Yehova wa Agano la Kale alikuwa tu Yesu wa Agano Jipya. Na—na Dk. Scofield hapa, tunaona

neno lake *kubadilishwa kwa umbo*, tunaona neno *en morphe* katika Kiyunani, ambalo maana yake ni "kisichoonekana kilifanywa kionekane." Kitu ambacho hatuwezi . . . Tunajua kiko. Kingekuwa—hakiwezi kuonekana, walakini, tunajua kiko. Na alipobadilisha umbo Lake la *en morphe,* ambayo maana yake ni kwamba Yeye alijigeuza kutoka cha kimbinguni kuingia cha kawaida . . . Naye tu akabadilisha kinyago Chake.

27 Kwa maneno mengine ni kama mchezo wa kuigiza; Yeye alikuwa akiigiza. Katika—katika Uyunani walipobadilisha vinyago vyao, labda mchezo mmoja—mchezaji mmoja angalicheza sehemu kadha mbali mbali. Naye binti yangu (aliyeko humu) . . . Wamekwisha kuwa na—na mchezo wa kuigiza katika shule ya upili. Nao—mvulana mmoja, ninayemjua, alicheza yapata sehemu nne, ila angeenda nyuma ya mahali pa kuchezea na kubadilisha kinyago chake kusudi aje akamwigize mtu mwingine.

28 Basi, ukichukua unabii wa Agano la Kale kuhusu yale Masihi angekuwa, unaweza kuulinganisha na maisha ya Yesu, nawe utaona Yesu alikuwa nani hasa. Yeye hakuwa mtu tu wa kawaida, Yeye alikuwa Mungu, *en morphe*. Yeye alijigeuza kutoka—kutoka wa kimbiguni akawa na umbo la maumbile ya mtu; hata hivyo Yeye alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, amefunikwa na utaji wa mwanadamu, wa kimwili. Nawe tazama Agano la Kale.

29 Na—na—najua ninazungumzia kusanyiko lililochanganyikana usiku wa leo kutoka mahali mbali mbali ulimwenguni. Nasi tuko hapa kuchunguza; je, sisi tu—tunafanya nini? Nini—tu akina nani . . . Twaelekea wapi? Nini kinatendeka? Haya yote maana yake nini?

30 Na sasa basi, tunaona hapa kwamba kama ninyi wanaume na wanawake wa Kiyahudi . . . na marabii he—he—hekaluni, katika siku zilizopita, kama wangalichunguza Biblia, zile nabii, badala ya hayo mapokeo, wangalitambua Yesu alikuwa nani. Hawangalimwita Belizebuli kamwe; hawangalimsulubisha kamwe. Bali yote yalipaswa kutendeka; hiyo ni sehemu ya huo mchezo. Nao walipofushwa katika jambo hili.

31 Ni kama wengi wenu wanaume na wanawake hapa usiku huu, labda rika yangu ama wazee kidogo. Mnakumbuka hapa Amerika miaka mingi iliyopita—wale Wachina (ndugu yangu ambaye wamemjulishwa hapa sasa hivi, nilikumbuka hilo nilipokuwa nikizungumza naye), jinsi walikuwa . . . Wao hawangezungumza Kiingereza, nao wali—waliendesha kazi ya dobi. Na unaenda kwenye kiwanda cha dobi kusafisha nguo zako. Yeye—yeye dobi wa Kichina angechukua kipande cha karatasi na kukirarua kwa njia fulani. Wewe ungechukua sehemu moja ya kipande hicho; naye angechukua sehemu iliyobaki. Bali unaporudi kudai mali yako, vipande hivyo

viwili vya karatasi vilipaswa kuumana barabara. Na iwapo havikuumana barabara (haungalikiigiza hata kidogo, kwa maana yeye alikuwa na sehemu moja nawe ulikuwa na hiyo nyingine), na kama kililingana . . . Ndipo ulikuwa na haki kudai yaliyo yako. Ndiposa, una yaliyo yako ikiwa ulikuwa na hiyo sehemu njingine ya mkataba huo.

32 Ndivyo ilivyo usiku wa leo iwapo una ile sehemu nyingine ya mkataba. Mungu alipomrarua Mwanawe vipande viwili huko Kalvari, akauchukua mwili huo juu kwa ajili ya dhambihu, na akamtuma Roho Wake huku chini kwetu, ambaye wakati mmoja aliishi katika mtu, Yesu (Mungu yule yule ametiwa utaji usiku huu katika mfano wa Roho Mtakatifu), vipande hivyo viwili sharti viunganike; ndipo wewe ni sehemu ya huo mkataba. Mungu alifanya hivyo apate kujulikana vema zaidi na mwanadamu, alipojifanya mwanadamu.

33 Nilikuwa nikisoma hadithi miaka mingi iliyopita, na katika hadithi hii ilisemwa mfalme mkuu aliyekuwa mungwana . . . nimesahau jina lake sasa hivi. Sikufikiria ningesimulia hadithi hii. Labda ilikuwa ya kubuniwa, bali ina—inatuelekezea jambo ambalo linatupa msingi wa yale tunayotaka kusema.

34 Mfalme huyu, yeye alikuwa mfalme mwungwana sana na aliyependa raia wake sana, hata siku moja mbele ya wa—walizi wake na watu wa jamaa yake alisema, "Leo mnaniona kwa mara yenu ya mwisho kwa muda wa miaka mingi."

35 Nao walinzi wake na watu wake mashuhuri wakamwambia, "Mfalme mwema, mbona unasema hayo" Je, unaenda katika nchi—nchi ya kigeni mahali fulani kuwa mgeni?

36 Akasema, "La, mimi nitakaa mumu humu. Vema," Kasema, "mimi naenda kule nje miongoni mwa raia wangu. Nitakuwa mkulima. Nitakata kuni pamoja na mkata kuni. Nita—nitalima shamba na mkulima. Nitapogoa mizabibu na wale wanaopogoa mizabibu. Nitakuwa mmoja wao kusudi ni—nipate kufahamu vizuri zaidi wanayofanya. Nami nawapenda, nami nataka kuwajua zaidi kibinafsi. Wao hawatanijua mimi, walakini, nataka kuwafahamu kwa njia hiyo."

37 Na asubuhi iliyofuata wakati wajumbe wake . . . Watu wake wote walimwona—ama wale wote waliokuwa katika jumbe la kifalme—akiitoa taji yake na kuiweka juu ya kitini (kiti cha enzi) na kuvua joho lake, na kuvalia mavazi ya mkulima, na kuondoka kwenda miongoni mwa watu wa kawaida.

38 Sasa, katika hadithi hiyo dogo tunaona basi habari za Mungu. Wao walimwambia huyo mfalme, kasema, "Mfalme, tunakutaka wewe. Tunakupenda. Tunakutaka uzidi kuwa mfalme."

39 Bali yeye alitaka kuwa mmoja wao apate kuwajua vyema zaidi, wapate kumfahamu vyema zaidi, jinsi alivyo hasa. lngewaonyesha wazi yeye alikuwa nini hasa.

40 Na hivyo ndivyo Mungu alivyofanya. Yeye alijigeuza kutoka kwa Yehova Mungu akawa mmoja wetu, apate kuteseka, apate kuonja mauti, apate kujua jinsi uchungu wa mauti ulivyokuwa, na achukue adhabu ya kifo juu Yake. Yeye aliweka kando taji Ya—Yake na joho Lake na akawa mmoja wetu. Yeye alitawadhana miguu na—na—na watu wa kawaida. Yeye aliishi katika hema na watu maskini. Alilala m—mstuni na barabarani za mji pamoja na makabwela. Yeye akawa mmoja wetu apate kutufahamu vizuri zaidi. Nasi tukapate kumfahamu Yeye vizuri zaidi.

41 Sasa, nafikiri katika hilo, tunaona akijigeuza Mwenyewe, kile alichofanya, kama utaona, Yeye alikuja katika jina la wana watatu. Alikuja katika jina la Mwana wa Adamu, na katika la Mwana wa Mungu, katika la Mwana wa Daudi. Yeye alikuja kama Mwana wa Adamu. . . Naam, katika Ezekieli 2:3, Yehova, Mwenyewe, alimwita Ezekieli nabii, mwana wa adamu. *Mwana wa Adamu* maana yake ni "nabii." Alikuja hivyo kutimiza Kumbukumbu la torati 18:15, ambapo Musa alisema, Bwana, Mungu wako, atakuoandokeshea nabii miongoni mwenu kama nilivyo. Yeye hakujiita kamwe Mwana wa Mungu. Alijiita, Mwana wa Adamu, kwa kuwa ilimpasa kuja kulingana na Maandiko.

42 Unaona, ilimbidi kufanya hivyo vipande viwili vya karatasi iliyoraruliwa unabii wa Agano la Kale na tabia Yake Mwenyewe, kulingana kabisa. Kwa hivyo akaja kama Mwana wa Adamu, akaja katika umbo hilo.

43 Kisha tunaona, baada ya kifo Chake, kuzikwa na kufufuka, Yeye akaja kwenye siku ya Pentekoste kama Mwana wa Mungu—Mungu, Roho, katika umbo hilo, Roho Mtakatifu. Alikuwa akifanyaje? Alikuwa akijigeuza Mwenyewe, akijijulisha kwa watu Wake katika umbo tofauti. Kama vile Roho Mtakatifu, ambaye ni Mungu, alivyokuja kutenda katika nyakati za Kanisa kama Mwana wa Mungu, Roho Mtakatifu. Bali katika ule Utawala wa Miaka Elfu Yeye yuaja kama Mwana wa Daudi kuketi juu ya kiti cha enzi cha Daudi—Mfalme. Ilimpasa kuchukua kiti cha enzi cha Daudi; Yeye yumo kwenye Kiti cha Enzi cha Baba sasa. Ndiposa, Yeye alisema, "Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja Nami katika Kitu changu cha Enzi, kama nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika Kiti Chake cha Enzi." Kwa hivyo Yeye—katika huo Utawala wa Miaka Elfu atakuwa Mwana wa Daudi. Ni nini? Mungu yule yule wakati wote akibadilisha tu kinyago Cha—Chake.

44 Mimi kwa mke wangu, ni mume. Je, mliona ya kwamba yule mwanamke Msirofoinike alivyosema, "Unirehemu, Mwana wa Daudi!" Yeye. . . Hakumjali kamwe. Huyo hakuwa na haki ya kumwita hivyo; Yeye hakuwa na madai yo yote Kwake kama Mwana wa Daudi. Yeye ni Mwana wa Daudi kwa Wayahudi. Na sasa, Yeye alikuja. . . Bali alipomwita Yeye *Bwana* (Yeye

alikuwa Bwana wake), Basi akapata aliyoomba. Sasa, kama . . . Yeye alikuwa akijigeuza tu.

45 Naam, nyumbani kwangu mimi ni watu watatu mbali mbali. Nyumbani mwangu mke wangu ana haki kwangu kama mumewe. Binti yangu kule, yeye hana haki kwangu kama mumewe; mimi ni baba yake. Na mjukuu wangu pale, mimi ni babu kwake; kwa hivyo hana haki ya kuniita baba yake. Mimi si baba yake; Mwanangu ndiye baba yake. Mimi ni babuye, bali ningali mtu yule yule.

46 Naye Mungu, anayofanya, Yeye hujigeuza atakavyokuwa katika kizazi hicho, kujijulisha kwa watu hao. Na hilo ndilo tunalotaka kuona usiku huu: Mungu anapaswa kujijulisha kwa njia gani kwa watu hawa na katika wakati huu? Yeye hubadilisha kinyago Chake; hugeuza matendo Yake, bali Yeye habadilishi asili Yake. Habadilishi ha—hali Yake; Yeye hubadilisha tu kinyago Chake kimoja akachukua kingine. Yeye hufanya hivyo apate kujifunua Mwenyewe zaidi kwa watu, wapate kujua Yeye ni nani na yu nini.

47 Katika Waebrania 1 tunasoma: "Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwanawe, Yesu Kristo." Sasa, manabii, Yesu alisema (alipokuwa hapa ulimwenguni), walikuwa miungu. "Mnawaita miungu wale waliojiliwa na Neno la Mungu; na Maandiko hayawezi kutanguka," Yeye akasema, "Je! mnawezaje kumhukumu Yeye basi, na huku Ndiye Mwana wa Mungu?" Mnaona? Neno la Mungu hugawiwa kila kazazi vile—litakavyokuwa; naye Yesu alikuwa ndiye utimilifu wa unabii wote. "Katika Yeye ulikaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili." Ulikuwa ndani Yake.

48 Ndiye aliyekuwa katika Yusufu. Ndiye alikuwa katika Eliya. Ndiye aliyekuwa katika Musa. Ndiye aliyekuwa katika Daudi, mfalme aliyekataliwa. Watu wake mwenyewe walimkataa kama mfalme. Naye alipokuwa akiondoka kwenye—kwenye behewa, maskini mtu mdogo kiwete, akitambaa huku na huko, yeye hakupenda—serikali ya—yake, utaratibu wake; naye akamtemea mate. Naye mlinzi akachomoa upanga wake, kasema, "Nimwachie mbwa yule kichwa chake, aliyemtemea mate mfalme wangu?"

49 Na Daudi, labda bila kujua alichokuwa akifanya wakati huo, ila alikuwa na upako, naye akasema, "Mwacheni. Mungu amemwambia afanye hivi." Naye akakwea hicho kilima na kuulilia Yeresalemu, mfalme aliyekataliwa.

50 Mlitambua, miaka mia kadha baadaye, Mwana wa Daudi, akitemewa mate barabarani, naye alikuwa juu ya kile kilima (mlima ule ule) akitazama chini juu ya Yerusalemu, Mfalme aliyekataliwa, na kupasa sauti, "Yerusalemu, ni

mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja—kama vile kuku awakusanyavyo vifaranga wake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka?"

51 Yeye hakubadilisha hali Yake, maana Waebrania 13:8 ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Mungu alifanyika mwili kusudi afe apate kutukomboa kutoka dhambini. Hiyo ndiyo sababu alijigeuza akawa m—mtu.

52 Tunaona katika Yohana 12:20, Wayunani walisikia habari Zake. Naam, hamna mtu awezaye kusikia habari Zake, mioyo yao isiwe inawasha—washa ipate kumwona Yeye. Kama vile Ayubu na manabii wa kale, wote walitaka kumwona Yeye. Kwa hivyo Wayunani wakaja kumwona. Wakamjia Filipo, aliyekuwa wa Bethsaida, na kusema, "Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Hao Wayunani walitaka kumwona; bali hawakuweza kumwona kwa sababu Yeye alikuwa katika hekalu la ubinadamu Wake. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake.

53 Sasa, tunaona kwamba katika hili, hawa Wayunani hawangemwona. Na tazama maneno hasa Yesu aliyowaambia baadaye; Yeye alisema, "Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake." Kwa maneno mengine, hawangeweza kumwona kamwe katika hilo badiliko, katika kinyago alichokuwa nacho wakati huo, kwa maana alikuwa amefunikwa katika mwili wa kibinadamu. Bali Chembe hii ya Ngano ilipoanguka katika nchi, ndipo itayaleta mataifa yote. Yeye alitumwa kwa Wayahudi, bila shaka, wakati huo, bali Chembe hii ya Ngano haina budi kuanguka. Mungu aliyetiwa utaji katika mwili wa binadamu, aliyefichwa kutoka kwa wasioamini, bali anafunuliwa kwa waaminio.

Katika Yohana 1:

> *Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu,*
>
> *Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, nasi* tukamwona Yeye . . . *Mwana pekee atokaye kwa Baba amejaa neema . . .*

54 Sasa, hapo mwanzo kulikuweko Neno. Neno ni wazo lililotamkwa. Hapo Mwanzo Yeye hata hakuwa Mungu. Sasa, neno letu la Kiingereza leo, *Mungu,* maana yake ni "kitu cha kuabudiwa." Inatatanishaje bongo. Unaweza kumfanya mtu fulani mungu. Unaweza kufanya cho chote mungu. Bali katika Agano la Kale, katika Mwanzo 1, *Hapo mwanzo Mungu . . .* neno linalotumiwa ni *Elohim. Elohim* maana yake ni "anayedumu Peke Yake." Jinsi neno *Elohim* lilivyo tofauti na neno letu *mungu. Elohim* maana yake ni "anayedumu Peke Yake."

55 Sisi hatu wezi kudumu peke yetu. Hatuwezi kuwa mwenye enzi; mwenye nguvu zote, anayeenea mahali pote, ajuaye yote. Neno *Elohim* hudhihirisha hayo yote. Hatuwezi kuwa hivyo. Huo

mti unaotengeneza mungu kwake, ama hilo—ama hilo jengo, havidumu peke yake.

56 Kwa hivyo Mungu, hapo mwanzo alikuwa Uzima, Aliye wa Milele. Ndani Yake mlikuwemo sifa, na sifa hizo zikafanyika maneno, nalo Neno likafanyika mwili. Yesu alikuwa Mkombozi. Na *kukomboa* maana yake ni "kurudisha." Na kusudi ikarudishwe, ilipaswa kuwa ilitoka mahali fulani itakaporudishwa. Kwa hivyo, unaona, watu wote hawataweza kamwe kuiona, kwa maana watu wote hawakuweko hapo mwanzo katika mawazo ya Mungu. Mwaona?

57 Watazame hao makuhani! Walipomwona akijitambulisha hasa na Neno alivyokuwa, wao walisema, "Ni Belizebuli." Hiyo ilionyesha asili yao ilimokuwa; ilikuwa katika mawazo mamboleo ya siku hizo. Bali yule maskini kahaba, aliyekutana naye mle langoni, na kumwambia—akaonyesha ishara Yake ya Kimasihi kwa kumwambia aliyokuwa ametenda, naam, yeye alisema, "Bwana, naona ya kuwa u nabii! Twajua Masihi; atakapokuja, Yeye atatuambia mambo haya yote." Yeye alikuwa akimtambua kama ndiye Masihi, Aliye na upako, kwa maana Yeye alitimiza masharti ya Maandiko. Je, hamwoni? Zile sehemu mbili za karatasi ile zilikuwa zikiunganika. "Tunajua ya kuwa atakapokuja Masihi . . . "

58 Sasa, huenda ilimlazimu Mungu kuunganisha *hiki* na *kile* kupata huu mlio fulani wa kengele, kama mfinyanzi, bali Yesu alipogeuka na kusema, "Mimi ninayenena nawe, Ndiye," hapakuwepo matamshi kama, "Belizebuli." Akauacha mtungi wake, akakimbia mjini, na kusema, "Njoni, mtazame mtu aliyeniambia mambo yote niliyotenda. Je! haiyamkini huyu kuwa ndiye Masihi?" Mwaona?

59 Sasa, kile kilichofanya hivi, kule kuweka Maandiko ya kale pamoja na ujuzi ambao Yesu alikuwa akimpa, kulifanyaje? Kulimfanya Masihi. Na ulitambua? Upesi, dhambi zake zilisamehewa, kwa maana hapo mwanzo yeye alikuwa anayeweza kukomboleka; kwa maana alikuwa katika mawazo ya Mungu hapo mwanzo. Kwa hivyo ilimkomboa, ama kumrudisha, alipoona Maandiko yaliyotamkwa yakimdhihirisha ya Yehova: jinsi Yeye alivyokuwa; jinsi Yeye alivyo.

60 Basi Yesu alipokuja, kama angalikuja na ujumbe wa Nuhu, haungalifaa kitu: kujenga safina na kuifanya ielee. Haungalifaa kitu. Lakini basi—Nuhu alikuwa sehemu ya Mungu. Yeye alitenda kwa njia ya kigeni, kwa sababu alikuwa mtu wa kipekee. Na ujumbe wake ulikuwa wa kipekee, kwa sababu ulikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa. Yeye hangalikuja na ujumbe wa Musa, kwa sababu ha—haugalifaa kitu. Musa alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa kwa sehemu; yeye alikuwa Neno lililonenwa kwa wakati huo.

Bali Yesu hangalikuja hivyo. Biblia haikusema angalikuja hivyo. Bali alipokuja jinsi hasa A—Agano lilivyosema angekuja, basi wote ambao wangekomboleka waliamini; kwa maana wao walikuwa mawazo ya Mungu. Zile sifa Zake hapo mwanzo zilifanyika mwili na zinazoweza kukomboleka, nao wakarudishwa kwa Mungu. "Wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu," kwa maana wangekomboleka. Wao walikuwa tangu mwanzo katika neno.

61 Kama tungalikoma hapa kwa muda mfupi (ikiwezekana) na tuwazie hilo usiku wa leo, juu ya ujumbe wa wakati huu, mawazo yaliyonenwa ya Yehova . . . Kabla misingi ya dunia, tunaambiwa majina yetu yaliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana—Kondoo. Ndipo tunaweza kuona pande hizo mbili, kama nilivyosema hapo mwanzo kwa nini mmoja ni wa kipekee kwa mwingine. Haina budi kuwa hivyo ilikuwa hivyo daima; imekuwa hivyo daima na itakuwa hivyo. Yeye alikuwa Neno, Naye Neno akafanyika mwili, akakaa kwetu.

62 Sasa, Mungu katika—kule nyuma katika siku za Agano la Kale tunaona ya kwamba baada ya kuwatokea watu Wake katika maumbo tofauti, Yeye alijitia utaji wa ngozi za pomboo—Mungu, akijificha nyuma ya ngozi ya pomboo kwenye kiti Chake cha rehema. Tunaona (jinsi Suleimani, alipoliweka wakfu hekalu la Bwana, na ngozi hizi za pomboo zilikuwa zimening'inia pale, ile pazia)—jinsi Yeye alivyoingia kama Nguzo ya Moto na kama Wingu, na akashuka na kwenda nyuma pale, na kujificha kutoka kwa ulimwengu wa nje. Bali kwa imani Israeli walijua Yeye alikuwa nyuma kule. Walijua Yeye alikuwa pale, haidhuru wo wote wa ulimwengu wa wapagani ungesemaje. Yeye alifichwa kwa asiyeamini, bali muumini, kwa imani, alijua kuwa Yeye alikuwa nyuma kule; walipata rehema. Naye alikuwa kwenye kiti Chake cha rehema, ambayo ilikuwa ni siri kuu.

63 Mnajua, katika Agano la Kale kuingia nyuma ya hiyo ngozi ilikuwa mauti. Sasa, kutoingia nyuma yake ni mauti. Wakati huo, kuingia katika utukufu Wake ilikuwa mauti, sasa, kutoingia katika utukufu Wake ni mauti. Hiyo ilitendeka, bila shaka, wakati lile pazia la hekalu lilipopasuliwa kule Kalvari, lile pazia lilipopasuliwa, lile pazia la kale. Kukaa nje ya uwepo Wake ni mauti. Wakati huo, kuingia katika uwepo Wake ilikuwa mauti. Mwaona? Inabadilika mbele nyuma, nawe huna budi kupata Maandiko kuona tunaishi wakati gani.

64 Sasa, lile pazia lilipopasuliwa Kalvari, kile Kiti cha Rehema kikaonekana dhahiri, lakini nini kilitendeka? Kilikuwa kinanig'inia Kalvari, kikitiririka Damu, kama vile walivyochukua damu mwaka baada ya mwaka wakati wa kutakaswa kwa patakatifu na kunyunyiziwa kwa Kiti cha Rehema, na pale, Mungu, kwa kupiga Kwake kukuu kwa nguvu za umeme, akapasua hiyo pazia ya kale ya pomboo toka juu hata chini, nacho Kiti cha Rehema kikaonekana

dhahiri. Yule Mwana—Kondoo halisi na wa kweli wa Mungu alikuwa akining'inia na kuonekana dhahiri kule Kalvari, kile Kiti halisi cha Rehema, Mungu Mwenyewe alipokwisha kulipia gharama na kuwa mmoja wetu, na alikuwa ameisha jidhihirisha Mwenyewe kama mwanadamu apate kutufahamu sisi nasi tupate kumfahamu Yeye.

65 Kiti cha Rehema kilionekana wazi mbele za Israeli wote katika hiyo siku ya Upatanisho. Lakini ole wangu! Mapokeo ya wazee wa kanisa siku hizo yalikuwa, kwa mapokeo yao, yalikifunika kwa pazia kile Kiti cha kweli cha Rehema kutoka kwa watu. Kama wangaliyajua Maandiko, kila sehemu yake ingalilingana kama kile kipande cha karatasi cha Wachina. Unabii wa Agano la Kale ungalitimizwa, na ulitimizwa. Na kama wangalikuwa wamefundishwa Maandiko, wao wangalikiona hicho Kiti cha Rehema.

66 Kama Musa alivyosema hapa ya kwamba. . .Hata hivi leo wametiwa utaji. Ungali umo mioyoni mwao; hawakioni. Bali Yeye alikuwa Mungu, kule kuona maumivu na huo Upatanisho. Yeye alikuwa kiti cha rehema halisi kilichoonekana dhahiri.

Kama tunavyouimba ule wimbo.

> Lo! mtazame akionekana dhahiri,
> Ndiye huyo, yule mshindi mwenye nguvu nyingi,
> Kwa maana alipasua ile pazia vipande viwili.

67 Mwaona, Yeye alikuja kama Kiti cha Rehema, akining'inia wazi mbele ya makutano. Bali wao wakiwa chini ya mawazo yapendwayo na watu wengi. . .Sasa, wanaume na wanawake, na wajumbe wa mkutani huu, nataka kusema hili, bila upendeleo. Lakini kwa ajili ya leo, kwa ajili ya kile kilichotuleta hapa leo, nachelea ya kwamba mapokeo ya wazee, wazee wa kanisa, yamelificha hili kutoka kwa watu wengi sana. Tangu Roho Mtakatifu alipokuja katika siku hizi za mwisho kama ilivyotabiriwa, na pazia imepasuliwa, watu wengi sana wanajaribu kudumu kwa mapokeo ya wazee; na hiyo ndiyo sababu hawawezi kuona hii raha kuu sana pamoja na amani, na mambo ambayo kanisa liliyo nayo siku hizi. Bali inaonekana wazi kwa wale waaminio. Yeye alilificha Neno, Neno lililoahidiwa la siku hizi.

68 Naam, hayo mapokeo yamesababisha huo utaji. Wao wanasema ya kwamba siku za miujiza zimepita. Mtu fulani alinizungumzia, muungwana mzuri, mwenye uungwana, kule Tucson, Arizona, ninakoishi. Nilikuwa nishakuwa na mkutano katika Ramada; nasi tulikuwa tukihubiri katika mkutano wa Wafanyi Biashara, ambapo Bwana Yesu alijitokeza na kutenda mambo makuu. Naye huyu Mkristo mungwana akanijia na kusema (mhudumu wa kanisa, mtu mzuri), naye akasema, "Ndugu Branham, unajaribu kuwaingiza watu katika wakati

wa kimitume," akasema, "na huku wakati wa kimitume umekwisha."

69 Nami nikasema, "Nakusihi wewe, Ndugu, unionyeshe lini wakati wa kimitume ulipokoma katika Maandiko." Nikasema, "wakati wa kimitume ulianza katika siku ya Pentekoste, na . . . Petro alisema kwenye siku ya Pentekoste, 'Ahadi hii ni kwa kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.' Je, ulikoma lini? Iwapo Mungu yungali anaita, basi wakati wa kimitume ungali unaendelea."

70 Na kwa hivyo, hapo ndipo watu hujaribu kuwafungia kitambaa machoni watu wengi sana, kwa mapokeo yao ya wazee, kama ilivyokuwa wakati huo. Nawe unakosa kuona kwa nini watu wemejaa sana furaha na shauku. Na mikutano hii ni ya kipekee sana, jambo geni sana kwa watu wengine ni kwa sababu wao wanaona. Wao walivunja vizuizi hivyo; wakapasua pazia hizo na kuingia katika uwepo wa Mungu ambapo wanaona ahadi ya Mungu iliyodhihirishwa ya wakati huu ikidhihirishwa mbele za watu. Wao wanaona yale Mungu aliyoahidi.

71 Katika Yoeli 2:28, Yeye aliahidi ya kwamba katika siku hizi za mwisho kungekuweko mvua ya vuli itakayomwagwa juu ya watu katika siku za mwisho. Nafikiri neno la Kiyunani hapo ni *Kenos,* ambalo maana yake ni "Yeye alijimwaga kabisa," si kama vile tungesema kitu fulani kilikuwa ndani ya mtu fulani kisha kikatolewa, bali kwamba Yeye alijimwagilia Mwenyewe kwao. Yeye alibadilisha *en morphe* Yake. A—akabadilika kutoka *alichokuwa* hata *alicho* sasa. Yeye habadilishi hali Yake kamwe.

72 Bali katika siku ya Pentekoste Yeye alijibadilisha kutoka Mwana wa Adamu akawa Mwana wa Mungu. Yeye alikuja, si *pamoja* na watu, bali *ndani* ya watu, waona, Mungu yule yule kuendeleza huduma Yake kupitia wakati huu ulio mkuu. Yeye alitabiri katika Biblia ya kwamba kutakuweko siku ambayo si mchana wala usiku, lakini wakati wa jioni kutakuweko nuru. Sasa, jua, kigeografia, hupambazuka mashariki na kutua magharibi. Ni jua lile lile wakati wote.

73 Basi, Mwana, (M-w-a-n-a,) alipojifunua katika dhihirisho la Neno lililoahidiwa Israeli, hao watu wa huko Mashariki . . . Tumekuwa na siku yenye utusitusi. Tumekuwa na nuru kutosha katika wale warekebishaji na kadhalika kuunda makanisa na madhehebu, na kujiunga nayo; na kuingia ndani yake na kuwabusi watoto wachanga; na kuoza watu wazima; na kuzika maiti, na kadhalika; na kuishi kanisani. Bali wakati wa jioni, "kutakuweko nuru," Yeye alisema, "wakati wa jioni." Na hakuna Andiko linaloweza kutanguliwa. Na M-w-a-n-a yule yule aliyejimwaga Mwenyewe, *Kenos,* katika siku ya Pentekoste, aliahidi kufanya jambo lile lile wakati wa jioni Mwaona? Ni kulingana na ahadi.

74 Unganisha hicho kipande. Tazama yanayotendeka, na utazame yale aliyoahidi, basi utaona mahali tulipo. Unganisha kitu hicho. Unaweza kuona kufunuliwa Kwake Huyu mkuu na aliye mwenye nguvu nyingi. Mapokeo yamewapofusha watu tena wasione mambo haya makuu ambayo yametabiriwa.

75 Musa, alipojitokeza kutoka mlimani, ambao ulikuwa ukiwaka moto. . .Jinsi mfano huu ulivyo mzuri. Musa alikuwa ameshuka kwenda Misri na kuwaambia wale wazee wa kanisa ya kwamba Mungu alikuwa amemzuru katika jina la MIMI NIKO. Jina hilo ni la wakati uliopo, si nilikuwa, nitakuwa, bali MIMI NIKO, yeye yule daima, yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye ni wakati uliopo. Yeye. . .Hiyo inalingana na Waebrania 13:8: "Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele."

76 Lingali ni Neno lililotabiriwa, na makutano waliopaswa kuandamana na hilo Neno, tukio la siku hizi. . . "Warekebishaji walikuwa nalo." Lo, lakini huu ni wakati mwingine. Oneni ni siku gani tunayoishi!

77 Jinsi tu Yeye hangalikuja katika siku alizokuja duniani, jinsi Musa alivyokuja ama ye yote wa manabii alivyokuja; haikuwa imetabiriwa. Na katika hizi siku za mwisho, imetabiriwa kuja hivi. Haiwezi kuja katika mfano wa ufufuo wa Luther, haiwezi kuja katika mfano wa ufufuo wa Wesley; ni wakati wa matengenezo. Ni wakati ambapo haina budi kurudia ile nuru ya asili, ya asili.

78 Lo, jinsi tungaliyalaza Maandiko juu yake! Nanyi wanatheologia (haidhuru mmetoka upande gani wa ulimwengu), mnajua ya kwamba hayo ni kweli. Ni ahadi. Hiyo ndiyo huwafanya watu wawe wa kipekee sana. Hiyo ndiyo huwafanya wawe watu wa kuchekesha sana kama mnavyowaita; ni kwa sababu wao wana. . .Ni. . .utaji umeondolewa kutoka kwa mapokeo, nao wanaiona. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ni—ni ahadi ya Mungu, na hatuwezi tukaenda dhidi yake, maana Maandiko hayawezi kutanguliwa.

79 Naam, twaona ya kwamba Yeye aliahidi ya kwamba angejimwaga Mwenyewe ndani ya watu Wake, naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

80 Musa, baada ya kushuka kwake kwenda Misri nakutangaza hili, ndipo Baba alithibitisha ujumbe wake kwa kushuka juu ya Mlima Sinai katika Nguzo ile ile ya Moto na kuuwasha moto huo mlima. Je, tulitambua yeye yule aliyempa ahadi? Yeye alimleta akiwa na Neno. Yeye alikuwa na zile amri, na ili apate hizi amri, ilimbidi ku. . .

81 Hizo amri zilikuwa Neno; Neno halikuwa limewajilia watu bado. Kwa hivyo Neno kila mara huja kwa nabii, naye alikuwa nabii kwa wakati huo.

82 Kama vile Yesu alivyokuwa Neno; Yohana alikuwa nabii, Naye Yesu akamjia majini, kwa sababu Neno humjia nabii bila

kukosea. Neno humjia . . . Kwa hivyo Musa, Neno lilimjilia, zile amri, naye alikuwa nazo.

83 Naam, basi, kabla Neno halijatolewa na kudhihirishwa, ilimbidi Musa kutia utaji juu ya uso wake, kwa maana Neno halikuwa limedhihirishwa kabisa. Walijua jambo fulani tayari lilikuwa limetendeka, bali hawakujua ilikuwa nini (kule kunguruma na mishindo ya ngurumo), hata wao wakasema, "Hebu Musa asema nasi na sio Mungu."

84 Naye Mungu akasema, "Vema, nitafanya hivyo. Tangu sasa sitawatokea hivi tena. Nitawatumia nabii. Kwa hivyo yeye . . . Nitanena kupitia nabii wangu."

85 Basi, kama Musa akiwa na torati ya kawaida (kama vile Paulo hapa katika II Wakorintho ametufunulia) ilimlazimu kutia utaji juu ya uso wake, zaidi sana ya Rohoni itakuwa yenye utukufu na iliyotiwa utaji kwa wasio amini kabla haijadhihirishwa kwao! Mara ngapi zaidi watakavyoita . . . ! Musa alikuwa mtu wa kipekee. Watawaita mara ngapi zaidi, nyinyi mliovunja huo utaji, mmeingia katika Nguzo ya moto na mkatoka na baraka! Na sasa mmekwisha kutiwa utaji! Watu hawawezi kuiona. Hawawezi kuifahamu. Kama ya kawaida yana utukufu, mara ngapi zaidi ya kimbinguni itakavyokuwa! Ikiwa ya kawaida, ambayo ilikuwa na mwisho, ingekuwa na utukufu, mara ngapi zaidi hii isiyo na mwisho itakuwa na utukufu!

86 Bali ingali imetiwa utaji. Imetiwa utaji si kwa muumini, bali kwa asiyeamini; hawezi kuiona. Mungu daima hujitia utaji kwa asiyeamini. Mapekeo huificha. Kama yalivyofanya wakati huo, yamefanya hivyo leo. Huo ulikuwa utaji wa kiroho tulio nao leo, ambapo mlikuwa na utaji wa kawaida. Ukithibitishwa na nabii kwa Neno lililoandikwa, mtabiri, mtu anayekuja na Neno lililoandikwa kulifanya dhahiri, walijua Neno lilikuweko, bali hawakujua maana yake; na Musa akalifanya dhahiri. Alisema, "Torati inasema *hivi*, na hii ndiyo sababu yake." Akalifanya dhahiri. Na kabla halijafanywa dhahiri, lilikuwa limetiwa utaji. Na ndivyo ilivyo siku hizi, limetiwa utaji kwa watu hata litakapofunuliwa na kufanywa dhahiri kwa watu—Mungu, Mungu Mwenyezi, ametiwa utaji katika mwili wa kibinadamu, lile Neno.

87 Tazama. Sasa, tunaona ya kwamba ilifichwa kwa asiyeamini, bali ikafunuliwa kwa anayeamini. Tazama. Ilimbidi Musa aingie katika hii Nguzo ya Moto peke yake; hamna mtu angalienda pamoja naye. Haikuwa . . . Hiyo . . . Hiyo inatuonyesha nini? Ya kwamba huingii humu kwa kujiunga na kundi la Kipentekoste. Unaona? Yeye hakulifunulia kamwe kikundi fulani; yeye alilifunua kwa mtu binafsi. Na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Unasema, "Mimi ni mfuasi wa ka—kanisa. Mi—mimi mshiriki wa hili." Bali hiyo haitafaa kitu. Unaona? Na kwa

ye yote kujaribu kumfuata Musa, kuigiza ilikuwa ni mauti. Na ndivyo ilivyo siku hizi, mauti ya kiroho kujaribu kuigiza. Hivyo ndivyo . . .

88 Usiku wa leo tunafikia kuinuka miongoni mwa makundi, kujilinganisha kwa kimwili—mtu akijaribu kutenda kama hiyo na kuishi maisha tofauti: anaweza kunywa pombe; anaweza kuvuta sigara; wanawake wanaweza kuishi vyo—vyo vyote watakavyo, na kama waliwengu; na kukaa nyumbani kutazama televisheni, na—na mambo ya ulimwengu, na hata hivyo kujiita Wapentekoste. Wao wanajaribu kuiga jambo fulani halisi. Haijafunuliwa kwao bado. Inapofunuliwa, ina utukufu na kitu fulani hutoa hayo kwako unapoingia mle. Unakuwa utaji. Ha—ha—haifai kitu. Na kuiiga ilikuwa mauti.

89 Musa akiwa ametiwa utaji, yeye alikuwa Neno lililo hai kwa watu. Na siku hizi, watu waliotiwa utaji ni jambo lile lile; wao ni barua zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote, si barua mpya, bali barua ambayo tayari imekwisha kuandikwa, ikadhihirishwa. Ni—ni wale wanaoamini Neno na ahadi ya siku hizi ambazo Mungu anawamwagia Roho Wake watu wote; na hao ndio barua zilizoandikwa. Na mtu anapojaribu kuiga hayo kimwili, haifui dafu. Maisha yako huonyesha ulivyo wewe.

90 Siku moja kulikuweko mvulana mmoja; aliyeingia katika shida fulani. Yeye alikuwa m—mvulana mzuri, bali a—akaenda mahakamani; naye hakimu akasema, "Nimekupata mwenye hatia. Sina budi kukuhukumia kifungo cha maisha."

91 Yeye akasema, "Nataka kuamua kesi yangu mwenyewe." Akasema, "Nataka iamuliwe kulingana na rekodi ya maisha yangu."

92 Hakimu akasema, "Hauna rekodi. Hata rekodi yako ndiyo inayokuhukumu."

93 Na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Sababu ambayo imefanya kanisa lisifaulu kama lipaswavyo kuwa, ni rekodi yake, ni maisha yake. Hatuna budi kuwa watu waliojitolea zaidi. Hatuna budi kuamini kila Neno la Mungu. Hatuna budi kutafuta hata Neno hilo litakapofanywa dhahiri kwetu. Mnaona? Rekodi ndiyo inayotuzuia kuingia.

94 Lakini wakati mmoja (kuwafanya mtoke katika kitanzi hiki) katika mahakama yaya haya, huyo mvulana hakuwa na fedha. Hangalilipa faini. Hi—hiyo faini ilikuwa imefikia dola elfu kadha. Bali alikuwa na nduguye mkubwa aliyekuja na kumlipia yote.

95 Sasa, sisi tuna Ndugu yetu mkubwa, Yesu, Mwana wa Mungu; Naye alikuja kutulipia, iwapo tu tutaamini na tuweze kuingia katika pazia pamoja Naye. Kama alivyo Musa wetu—Yesu ni Musa wetu siku hizi; Musa aliyetiwa utaji alikuwa Neno linaloishi kwa watu. Siku hizi, Yesu aliyetiwa utaji ni Neno lililo hai kwa watu ambao . . . Yesu kanisani. Roho Mtakatifu, Mwana

wa Mungu, ndani ya watu, akilifunua Neno kwa ahadi ya leo, akilifanya halisi hasa. Yule yule sasa!

96 Na kumbuka, Musa alifanya hili na kudhihirisha hili, si kwa ulimwengu mzima, bali kwa watu wa kule kutoka—tabaka moja tu ya watu. Hao walikuwa wale waliotoka nje ya—katika kule kutoka. Na siku hizi, Roho Mtakatifu, mbele ya wale watu wasemao "Uponyaji wa kiungu si wa kweli!"...Nilipokuwa nikishauriana...

97 Daktari alinipigia simu hivi majuzi juu ya maskini bibi mmoja...Lo, kumekuwa na wagojwa wanne watano pale, kwenye ghari ya mauti wamepewa masaa machache, na Roho Mtakatifu akawaponya. Huyo daktari alikuwa akiswali hilo, akasema, "Hii yawezekanaje? Kwa nini," akasema, "ni—ni... Huyo ni mgojwa wangu."

98 Nikasema, "Alikuwa wako, bali sasa ni wa Mungu. Ni—ni—ni mtu Wake sasa." Unaona?

99 Na kwa hivyo, unaona jinsi ilivyo, ya kwamba Mungu anaita watu waondoke kutoka nyuma ya pazia ya kimwili wanaojaribu kuiga, wanaojaribu kujiunga na kanisa, si Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbeteria peke yao, bali makanisa ya Kipentekoste. Ni jambo la mtu binafsi; ni wewe na Mungu. Huna budi kuingia, si kundi lako, si kanisa lako, si mchungaji wako, bali ni wewe unayepaswa kuingia.

100 Nataka muone tabia nyingine ya Musa. Alipotoka, ingawa alikuwa—nabii, akiwa mtu mkuu jinsi alivyokuwa, alipotoka akiwa na Neno, watu waliona ya kwamba alikuwa amebadilika. Kitu fulani kilikuwa kimetendeka kwake. Alipotoka akiwa na Neno lililothibitishwa la wakati huo, zile Amri, yeye alikuwa mtu aliyebadilishwa. Na ndivyo wewe utakavyokuwa utakapotoka nyuma ya huo utaji wa kibinadamu ambao ungecheka mkutano kama huu, huyo mtu ambaye angekwazwa na uponyaji wa Kiungu, na kusema, "Siku za miujiza zimepita."

101 Wewe jitoe kutoka kwa huo utaji wa binadamu hapo, utaji wa mapokeo, na kila mtu atajua ya kwamba jambo fulani limetendeka kwako.

102 Kama Ndugu yetu mwaminifu Jim Brown, nakisia karibu Wapresbeterian wote au—wanajua jambo fulani lilitendeka kwake kwa maana alitoka nyuma ya utaji wa mapokeo. Yeye aliona kitu katika watu hao kilichomvutia, naye akatoka nyuma ya huo utaji. Vema, wewe...unapotoka nyuma ya huo utaji, utaonekana wazi wazi na watu, wapate kuona kwamba jambo fulani limetendeka kwako. Neno lililotiwa utaji kwa asiyeamini, bali wazi kabisa kwa muumini: Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.

103 Basi ilikuwa Mungu...Siki hizo ilikuwa Mungu katika mtu, Mwanawe, Yesu Kristo. Tunaamini hilo. Si nabii tu, si mtu wa kawaida tu, mwanadamu wa kawaida, ilikuwa ni Mungu katika

Kristo, Mungu, katika mtu, utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili katika mtu. Mungu, katika mtu; sasa, ni Mungu katika watu. Mnaona? Utimilifu wa Mungu katika Uunga kwa jinsi ya mwili katika Kanisa Lake lote, akijidhihirisha Mwenyewe, akitimiza Neno Lake.

104 Sasa, tunaona, Mungu katika nyakati zote amekuwa na ngozi. Mwaona? Mungu amekuwa amefichwa nyuma ya utaji. Inanikumbusha tu juu ya—ya—hadithi dogo iliyotukia kule chini Kusini. Na kwa hivyo, kulikuwa na jamaa ya Kikristo. Na hii—katika jamaa hii ya Kikristo wao walimwamini Mungu, nao—wao walifikiri ya kwamba Mungu, aliwalinda kutoka kwa shida zote; Naye hufanya hivyo. Nao walikuwa na mdogo mmoja (mvulana mdogo yapate umri wa miaka saba au minane), na—naye alihudhuria shule ya Jumapili naye alikuwa mvulana mzuri sana; bali aliogopa sana dhoruba, zaidi sana wakati umeme unamemeteka.

105 Nilipomwambia mtu huyu hivi majuzi, wakati habari hizi zilitokea kuhusu kuponywa mtu huyu, huyu muhudumu alisema, "Wanakufanya mungu, Ndugu Branham."

106 Vema, yeye alikuwa mtoa lawama, kwa hivyo nikaamua ninge—ningeikatisha kidogo, si kumuumiza, mwajua, bali tu ni . . . Nikasema, "Je, hiyo iko mbali sana na Maandiko kuwa hivyo?" Unaona? Nikasema, "Sivyo, haiko mbali. Nikasema,' Kwa maana Yesu aliwaita manabii miungu." Unaona? Hiyo ni kweli. Mungu . . .

Nao husema, "Vema, nyinyi watu hujaribu kutwaa mahali pa Mungu."

107 Hilo haliko mbali sana, hivyo ndivyo ilivyo hasa. Hivyo ndivyo hasa! Mungu akidhihirishwa katika mwili, jinsi tu alivyoahidi.

108 Maskini jamaa hii, tunaona ya kwamba . . . Nalimhadithia hii hadithi ndogo (ambayo imeingia bongoni sasa hivi), ya kwamba usiku mmoja dhoruba ikaja, naye Mama kamwambia Mdogo, kasema, "Sasa, nenda orofani, Mwanangu, nenda kalale."

Yeye akasema, "Mama, naogopa sana." Akasema . . .

"Hamna kitakachokudhuru. Panda juu ukalale."

109 Maskini Mdogo yule akalala mle, huku umeme ukimemetesha madirishani, na maskini mtoto huyo akapatwa na wasiwasi mwingi sana. Yeye angekificha kichwa chake, bali angesikia hu—huo umeme—ama kuuona umeme ukimemetesha madirishani, na—na kusikia mishindo ya ngurumo; kwa hivyo akasema, "Mama!"

Naye akasema, "Unataka nini, Mdogo?"

Kasema, "Njoo humu ukalale pamoja nami!"

110 Kwa hivyo akapanda kwa vipandio kama mama mzuri na mwaminifu angalifanya; naye akaja, na kumshika maskini Mdogo mikononi mwake na kusema, “Mdogo, Mama anataka kunena nawe kwa muda mchache.”

Kasema, “Vema, Mama.”

111 Kasema, “Sasa, huna budi kukumbuka hili. Sisi huenda kanisani daima; tunasoma Biblia; tunaomba; sisi ni jamaa ya Kikristo; tunamwamini Mungu.” Na kasema, “Tunaamini ya kwamba katika dhoruba na yo yote yanayotendeka, Mungu ndiye ngao yetu.”

112 Yeye akasema, “Mama, naamini kila moja ya hayo, lakini,” kasema, “huo umeme unapokuwa karibu hivi,” akasema, “na—nataka Mungu aliye na ngozi.”

113 Kwa hivyo na—nafikiri, si Mdogo peke yake, bali sisi sote tunajisikia hivyo. Tunapokusanyika pamoja, tunapoombeana . . . Mungu aliye na ngozi.

114 Na tunaona ya kwamba Mungu daima amekuwa na ngozi. Musa alipomwona, Yeye alikuwa na ngozi; Yeye alionekana kama mtu. Mungu alipokuwa nyuma ya zile pazia, Yeye alikuwa na ngozi. Na Mungu, usiku wa leo, katika Kanisa Lake ametiwa utaji katika Kanisa Lake akiwa na ngozi. Yeye yungali Mungu yule yule usiku wa leo. Tunaona hayo.

115 Lakini sasa, kama kawaida, huo utaji wa ngozi ndio unaoyanasa mapokeo. Wao hawawezi kuamini ya kwamba huyo ni Mungu anayewafanya watu hao kutenda hivyo. Mnaona? Ni kwa sababu Mungu ametiwa utaji katika Kanisa Lake, katika ngozi—Yuna ngozi. Hiyo ni kweli. Yeye amefichwa kwa asiyeamini, na akafunuliwa muumini. Naam, bwana!

116 Naam, utaji wao wa mapokeo—wa—wa mapokeo ya wazee na Neno unapovunjiliwa mbali (lo, bila shaka, siku hizi), ndipo Yeye anaonekana dhahiri, sisi tunamwona Yeye, Umungu kwa mara nyingine tena umefichwa katika mwili wa mwanadamu. Waebrania 1 ilisema hivyo, na pia Mwanzo 18. Mnakumbuka Mungu alikuwa mtu, akisimama pale huku akila na kuzungumza na Ibrahimu, na kumwambia aliyokuwa akitenda Sara hemani nyuma Yake. Naye yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana wa Adamu,” Umungu kwa mara nyingine tena umefichwa katika mwili wa mwanadamu.

117 Sasa kumbuka, Yesu hakusema, “Atakapofunuliwa *Mwana wa Mungu,*” katika Luka sura ya 17, naamini, na yapata kifungu cha 20, 21, mahali fulani hapo; Yeye alisema, “Na wakati *Mwana wa Adamu* anapofunuliwa,” yule Mwana wa Adamu amerudi Ka—Ka—Kanisani tena, amefunuliwa katika wanadamu, si Mwana wa Mungu, bali Mwana wa Adamu tena, amerudi Kanisani Mwake tena katika siku za mwisho. Tunaona ya kwamba Yeye aliahidi hayo katika ahadi za Mungu.

118 Tunaona jambo jingine. Katika Agano la Kale (nina Andiko hapa katika Kutoka) ambapo zile ngozi za kale za pomboo. . . Zilifanya nini? Zilificha utukufu wa Mungu kutoka kwa watu— hizo ngozi za pomboo. . .Sababu ya watu wasiuone, ni kuwa ulifunikwa na ngozi. . .Ngozi ilikuwa. . .Utukufu wa Mungu ulikuwa nyuma ya hiyo ngozi. Na sasa, utukufu wa Mungu umo nyuma ya ngozi yako (hiyo ni kweli!), na mapokeo hayauoni. Umo ndani ya lile pazia ambamo Neno Lake lilikuwa.

119 Nini kilikuwa upande wa ndani wa ngozi hizo, kule nyuma, zile ngozi za kale za pomboo, ambamo hamkuwemo uzuri hata tuutamani? Na ulipofanyika mwili na ukaishi kwetu, haukuwa na uzuri bado hata tuutamani. Na sasa, ni jambo lile lile siku hizi. Hamna kitu ndani ya mwanauwe au mwanamke tunachoweza kutamani, bali ni kile kilicho nyuma kule. Hicho ndicho.

120 "Vema," unasema, "mtu huyo najua alikuwa mlevi. Alizoea kufanya *hivi*." Sijali aliyozoea kufanya. Nini kilichofichwa nyuma ya hiyo ngozi? Kile kilicho nyuma mle, ndicho muhimu, hicho ndicho. . .Watu wamepofushwa, hiyo ngozi huwapofusha watu. Mwaona? Wao wanasema, "Nakumbuka mwanamke yule alizoea ku. . . "

121 Najua aliyozoea kufanya, lakini sasa je? Mnaona? Hizo ngozi ndizo wakati mmoja zilikuwa kwenye hiyo pomboo, lakini sasa, zinaficha utukufu wa Mungu, umepata makao Yake nyuma yake. Ulikuwa juu ya mnyama, bali sasa, ni makao ya utukufu wa Mungu.

122 Vivyo hivyo ngozi yako inaweza kubadilishwa usiku wa leo, kufanywa makao ya utukufu wa Mungu, Mungu akifanya makao Yake katika jamii ya wanadamu.

123 Tazama, zile ngozi za kale za pomboo, tunaona kwamba nyuma yake mlikuwa—ndani mle mlikuwa Neno. Nalo Neno. . . Kulikuwemo pia ule mkate wa wonyesho. Lile sanduku la agano lilikuwa limenyunyiziwa. Na ilikuwa nini? Utukufu wa Shekina ulikuwa mle.

124 Sasa, Neno ni Mbegu, na haliwezi kuzaa hadi ju—jua liiguse. Jua halina budi kuwa juu ya mbegu kuifanya izae mazao, kuifanya itokee. Na hivyo tu ndivyo tu unavyochukua Neno. Unaona? Pokea Neno la Mungu moyoni mwako ukaingie katika utukufu wa Shekina. Na utakapofanya hivyo, italeta mana ya mkate wa wonyesho unaopewa tu watu waliotengwa. Kitu tu kinachoweza kuila, ambacho kimeruhusiwa kuila, ni watu tu wale ambao wameruhusiwa.

125 Na tazama, Paulo alisema hapa, "Tunabadilishwa toka utukufu hata utukufu." Unaona? Hatimaye ina—inarudia utukufu wake asili. Ni kama tu mbegu ya asubuhi. Mbegu ya ua, huanguka ardhini. Punje ya ngano huanguka ardhini. Kitu cha kwanza ni nini? Inaota, na ni chipukizi ndogo; kisha

inakuwa kishada. Halafu kutoka kwa kishada inarudia mbegu yake asili.

126 Vema, hivyo ndivyo hasa Kanisa limetenda. Lilitoka kwa Luther, Wesley, na sasa, limerudia ile punje halisi, likarudia utukufu Wake wa kwanza, kurudia utukufu lililokuwa nao hapo mwanzo. Jua lililopambazuka Mashariki ndilo jua lile lile linalodhihirisha jambo lile lile Magharibi, likibadilika toka utukufu hata utukufu.

127 Lilibadilika kutoka kafiri hata kufikia Luther, na kutoka kwa Luther kufikia Wesley, na kutoka kwa Wesley kufikia Pentekoste, na kuendelea mbele likibadilika kutoka utukufu hata utukufu, likizaa mana iliyofichwa. Na sasa limeiva lipate kumrudisha Yeye tena jinsi hasa Yeye alivyokuwa hapo mwanzo, huduma Yake, Yesu yule yule uweza ule ule, Roho Mtakatifu yule yule. Yeye liyeshuka katika siku ya Pentekoste ndiye Roho Mtakatifu yule anayedhihirishwa siku hizi, toka utukufu, hata utukufu, hata utukufu, na kurudia ile mbegu yake asili kwa Ubatizo wa Roho Mtakatifu, pamoja na ishara zile zile, ajabu zile zile ubatizo ule ule, watu wa aina ile ile wakitenda vile vile, wakiwa na uweza ule ule, mwamsho ule ule. Ni kutoka utukufu hata utukufu. Na hatimaye tutabadilishwa kutoka utukufu huu kuingia katika mwili Wake wa utukufu ambapo tutamwona Yeye. lbrahimu aliona uo huo.

128 Sasa, tazama. Tunaona jinsi ulivyobadilishwa. Tangu Kalvari tumekaribishwa kushiriki utukufu Wake. Sasa, katika I Wakorintho 12, “Tumebatizwa katika Mwili Wake.” Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa, si kwa maji mamoja, Roho mmoja sisi sote tumebatizwa. Hiyo ni kweli. Basi Na ndipo, tunakuwa sehemu Yake. (Natumaini siwakakawishi sana. Mnaona? Natumaini siwakawishi.)

129 Lakini ni kama tu muziki wa tarabu kubwa unaochezwa au kucheza mchezo wa kuigiza. Sijui mengi sana kuhusu muziki wa tarabu au michezo ya kuigiza, bali nilikuwa nikiutazama mchezo huu, nilikuwa nikinena juu ya, *Carmen,* wakati binti yangu na wengineo walipokuwa humo. Nao walikuwa wakicheza huu muziki wa tarabu, katika *Carmen*. Walikuwa wakiuigiza . . . muziki uli—uli—ulikuwa ukicheza jambo lile lile. Hivyo ndivyo ilivyo unapobatizwa na Roho Mtakatifu katika Kristo.

130 Sasa oneni, wengi wenu wamesoma ama kusikia hadithi ya yule mtungaji mashuhuri wa Kirusi aliyeutunga *Petro na Mbwa Mwitu*. Na jinsi yeye—wao waliuigiza huo kwa mifano na kila kitu. Ye yote anayejua hadithi hiyo, anayeisoma kwa kijikaratasi, na anaweza kusikia muziki huo wa tarabu, jinsi unavyoigiza, huo mchezo wa kuigizwa, ukichezwa, kwani, wao wanajua kila badiliko. Wao wanaweza kuangalia hapa na kuona badiliko. Bali sasa, inakuwaje kama—kama mtungaji huyo ataandika jambo fulani, na tunaona ya kwamba haliigizwi

vilivyo? Tunaona basi ya kwamba jambo fulani limetendeka, kuna kasoro fulani. Tunapo waona . . . Yeye aliyeutunga—kuutayarisha na kuuandika, ndiposa, wacheza muziki wa tarabu watoe sauti baya; kuna kasoro. Kiongozi aliashiria vibaya. Mwaona?

131 Na hiyo ndiyo shida siku hizi, ndugu zangu Walutheri ndugu zangu Wabatisti, ndugu zangu Wapentekoste, ndugu zangu wote kutoka madhehebu yote mbali mbali; hivyo ndivyo ilivyo. Mwaona? Mnajaribu kutoa sauti iliyotolewa katika siku za Luther, au Wesley, hivyo, huku—huku Karatasi ya Muziki hapa ikionyesha ya kwamba ni siku nyingine. Mwaona, mwaona? Hatuwezi kuishi katika nuru ya Luther; yeye alikuwa mrekebishaji. Tunathamini se—sehemu yake, bali hiyo tulicheza tukaimaliza. Tuko humu nyuma ya Kitabu sasa. Mnaona? Hatuwezi—hatuwezi kiucheza hivyo.

132 Sasa, njia pekee mtakayoweza kulifanya ndugu zangu, ni hii . . . Na ndugu zangu wa ulimwenguni (wa sehemu mbali mbali ulimwenguni, huenda nikasema), kuna njia moja tu kwa huyo—kwa huyo kiongozi kufanya. Hana budi kuingia katika roho ile ile alimokuwa mtungaji wa nyimbo wake, basi anafaulu. Na wakati Kanisa, tarabu yenyewe (ambapo ulimwengu unatazama hizi ishara ya maajabu), wakati Kanisa na Mtungaji, na kiongozi wote wakiingia katika Roho ya Mtungaji basi wanaposema, "Siku za miuzija zimepita," hawaimbi sauti ya kweli. Bali muziki unapofikia mdundo kweli—kweli na kuingia katika roho halisi yake . . . Utawezaje kufanya hivyo isipokuwa Roho ashuke kutoka kwa Mtungaji? Amina!

133 Ndipo unaposema, "Siku za miujiza hazijapita bado," tarabu inalia kwa sauti kuu, "Amina!"

134 Tunapopiga hivi, "Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele," tarabu inalia kwa sauti kuu, "Amina!"

135 "Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu"; tarabu inalia kwa nguvu, "Amina! Ninayo." Hamna tena kubahatisha kuhusu hayo wakati huo; tarabu yote ina ulinganifu na Neno. Inaenda tu [Ndugu Branham apiga makofi kueleza mfululizo wa mwendo ama mwendo mbali mbali wa muziki—Mh.]. Ndivyo. Lo, ni jambo tukufu sana. Kiongozi na Mtungaji hawana budi kuwa katika Roho yule yule, na pia wanamuziki hawana budi kuwa katika Roho yule yule wapate kuuigiza wote. Na ulimwengu unashangaa nini kinatendeka.

136 Huo ukomunisti, wanaonena habari zake—nao waniudhi kwake—na huu muungano, na mengine yote, na mtengano huu wote . . . Jamani, rehema! Hivi—upuzi huu wote hali kuja kwa Bwana kumewadia! Kuna kitu kinachopigwa vibaya. Nasikitika kiongozi ana—viongozi wametoka katika Roho ya Mtungaji.

137 Tunapopata Roho ya Mtungaji, ule uweza asili wa Mungu (ambapo Biblia ilisema watu wa kale waliongozwa na Roho

Mtakatifu kuandika Biblia hii), utaona ya kwamba hivyo vipande viwili vya karatasi ya Wachina vitaumana tu kama vile Biblia ya Mungu na muumini wataungana; kwa sababu hao wawili wamo katika Roho yule yule; hao ni kitu kile kile. Wanaunganika moja kwa moja.

138 Tunachohitaji siku hizi ni viongozi. Hiyo ni kweli. Rudi kwa Neno. Rudi na kuliamini jinsi tu lilivyosema.

139 Ndipo mnamwona Mungu, Mwenyewe, huko ni kufunuliwa; mchezo wa kuigiza unafanywa kweli. Siku hizi wao husema, "Vema, Yeye ni Mungu wa kihistoria. Tunajua alivuka Bahari Shamu. Alitenda haya yote, naye alikuwa katika—katika tanuru ya moto uwakao pamoja na wana wa Kiebrania." Mungu wa historia anafaa nini, ikiwa Yeye—ikiwa Yeye si yule yule leo?

140 Mwanadamu daima anamtukuza Mungu kwa yale Yeye aliyofanya, akitafakari yale atakayotenda, na anapuuza yale anayotenda. Hiyo ndiyo tabia ya mwanadamu kufanya hivyo, na ni jambo lile lile siku hizi, ndugu zangu; ni jambo lile lile.

141 Jamani! Na turudi tukaifanye tarabu icheze vizuri, ambapo walimwengu wanaweza kuona. Yesu alisema, "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote Kwangu." Na ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

142 Hebu na viongozi waingie katika Roho halisi pamoja na wanamuziki na pamoja na Mtungaji, kila kitu kitakuwa sawa. Ndipo tuna—hamna kubahatisha juu yake, tumeunganika Naye wakati huo. Waebrania 13:8. ilisema, "Ni yeye yule jana, leo na hata milele."

143 Tunaunganika Naye katika Matendo 2. Tunaunganika nao, kwa ubatizo ule ule, jambo lile lile. Yote aliyokuwa wakati huo na yote aliyo, yote Yeye aliyokuwa na yote aliyo, ndivyo tulivyo. Ndivyo hasa.

144 Kama vile, kama nikitaka kuwa Mwamerika kweli, sina budi kuunganika na cho chote ilichokuwa, cho chote ilicho. Sina budi kuunganika nayo, iwapo mimi ni Mwamerika kweli kweli. Iwapo mimi ni Mwamerika kweli kweli, basi nilishuka pwani ya Plymouth Rock. Amina! Nilifanya hivyo, iwapo mimi ni Mwamerika. Wewe pia; ulishuka pwani ya Plymouth Rock pamoja na wale baba wasafiri. Katika Playmouth Rock, waliposhuka pwani kule, nilikuwa pamoja nao; wewe pia, kila mmoja.

145 Nalipanda farasi pamoja na Paul Revere moja kwa moja barabarani kuwatahadharisha. Hiyo ni kweli hasa. Moja kwa moja hapa chini katika Valley Forge, nikavuka Delaware iliyojaa barafu pamoja na kikosi cha askari ambao nusu yao hawakuwa na viatu. Naliomba usiku kucha pamoja na George Washington hapo mbeleni. Nikavuka Delaware nikiwa na ona moyoni mwangu. Sisi ni Waamerika. Naam, bwana! Huko Valley Forge, bila shaka nilifanya hivyo.

146 Nalishukuru pamoja na wale baba wa kwanza walioshukuru; nikamrudishia shukurani Mungu. Kama mimi ni Mwamerika halisi. Mimi niliunganika pale mezani. Kama ni Mwamerika halisi niliunganika niliposimama na Stonewall Jackson. Iwapo mimi ni Mwamerika halisi, niliunganika katika Boston Tea Party (naam, Bwana!) tulipokataa kufungwa macho yetu. Wakati nilipokuwa Mwamerika halisi niliunganika hapo kwa hayo. Naam bwana! Jamani!

147 Nilipiga Kengele ya Uhuru tarehe 4 Julai 1776. Nilipiga Kengele ya Uhuru hapa na kutangaza ya kwamba sisi ni huru. Kusudi niwe Mwamerika kweli kweli ilinipasa kufanya hivyo. Niliunganika na ile aibu yake ya Mapinduzi, wakati ndugu alipigana dhidi . . . Sina budi kustahimili aibu yake jinsi tu inavyonibidi kustahimili utukufu wake. Iwapo mimi ni Mwamerika, sina budi kufanya hivyo. Niliunganika nayo. Naam, Bwana!

148 Niliunganika katika Gettysburg kule chini, wakati Licoln alipotoa hotuba yake. Naam, Bwana! Nilikuwa katika Kisiwa cha Wake, juu ya miili ya askari iliyolowa damu. Naliinuka katika Kisiwa cha Wake. Kule Guam, nikasaidia kupandisha ile bendera. Mimi ni Mwamerika kweli kweli. Amina! Yote iliyo, ndiyo niliyo mimi, na naona fahari kwake. Ndivyo, hasa! Yote Amerika imekuwa, yote iliyo, ningali hiyo kusudi niwe Mwamerika. Cho chote ilichokuwa, sina budi kuwa, sababu mimi nimeunganika nayo.

149 Ni jambo lile lile unapokuwa Mkristo wa kweli. Huna budi kujiunganisha nao. Nalihubiri pamoja na Musa na kuwa—pamoja na Nuhu na kuwaonya watu juu ya hukumu ijayo, kuwa Mkristo halisi. Nilikuwa pamoja na Musa katika kijiti kilichowaka moto; niliona ile Nguzo ya Moto; naliona utukufu Wake. Nalikuwa pamoja na Musa kule jangwani. Kuwa Mkristo, sina budi niunganike na cho chote Mungu alichokuwa, kuwa Mkristo. Niliona utukufu Wake, nilisikia sauti Yake. Usijaribu kuieleza vingine sasa, kwa maana nilikuwa huko. Ninajua ninayonena. Niliona kile kilitendeka. Naam, Bwana!

150 Nilikuwa katika Bahari ya Shamu nilipoiona Roho ya Mungu ikishuka na kutenganisha maji kutoka upande mmoja, si kupitia kwenye kundi la nyasi, wanavyojaribu kusema siku hizi, bali kupitia kwenye futi tisini za bahari. Nilimwona Roho wa Mungu. Nilitembea na Musa kupitia katika nchi kavu, kuvuka Bahari ya Shamu. Nilisimama karibu na Mlima Sinai na kuona ngurumo na umeme zikianguka. Nilikula mana pamoja nao kule. Naliunywea ule Mwamba; ningali ninafanya hivyo usiku wa leo. Naliunganika na wanaokula mana na hao waliounywea huo mwamba.

151 Naliunganika pia na Yoshua alipopiga tarumbeta na kuta za Yeriko zikaanguka. Nalikuwa katika tundu la simba na Danieli.

Nalikuwa katika tanuru iliyowaka moto pamoja na wale wana wa Kiebrania. Nalikuwa pamoja na mlima—pamoja na Eliya juu ya mlima Kermeli.

152 Nilikuwa pamoja na Yohana Mbatizaji na mbele zao hao wenye kulaumu. Nilimwona Roho wa Mungu akishuka; nilisikia sauti ya Mungu ikisema, "Huyu ni Mwanagu, mpendwa Wangu, ninayependezwa kukaa ndani Yake." Naam, bwana. Bila shaka niliunganika pamoja naye. Ndivyo hasa.

153 Niliunganika pale kwenye kaburi la Lazaro alipomfufua Lazaro. Niliunganika na yule mwanamke kisimani wakati Yeye alipomwambia dhambi zake. Naam, bwana! Bila shaka niliunganika Naye katika kifo Chake. Nami niliunganika kwenye ile Pasaka ya kwanza, nalifufuka pamoja Naye toka mle. Niliunganika Naye katika mauti Yake.

154 Nalikuwa pamoja na wale 120 Orafani. Niliunganika nao. Lo, na—najisikia wa kidini sana. Lo mie! Niliunganika pale. Mimi ni mmoja wao. Niliunganika; nina tukio lile lile walilokuwa nalo. Nalikuwa mle ilipotendeka, kuwa Mkristo halisi.

155 Nilishuhudia upepo wa nguvu ulioenda kasi ukija. Nilishuhudia huo. Nalisikia uweza wa Mungu ulipotikisa. Nilikuwa pamoja nao walionena kwa lugha. Nilisikia upako ukija mle. Nilikuwa pamoja nao. Niliunganika nao wakati Roho alipoanza kunena kwa lugha kupitia kwao. Nilikuwa pamoja na Petro mbele ya wenye kulaumu wake katika Matendo 2, alipohubiri mahubiri makubwa hata . . . Niliunganika naye. Naam, bwana!

156 Wakati Mitume 4, walipokusanyika pamoja, nilikuwa pamoja nao wakati jengo hilo lilipotikisika. Baada ya mkutano wa maombi jengo lilipotikiswa mahali walipokuwa wameketi; niliunganika nao hapo pamoja nao.

157 Nilihubiri na Paulo juu ya Areopago. Naam bwana! Nilikuwa pamoja na Yohana kwenye kisiwa cha Patmo na kuona kule kuja Kwake kwa pili. Nilikuwa pamoja na Luther katika yale Marekebisho. Nilikuwa pamoja na Wesley, huyo kinga kilichonyakuliwa miotoni, wakati ule uasi mkuu dhidi ya kanisa Anglikana; nalikuwa pale pamoja naye.

158 Nami nimo humu katika mwaka wa 1964, katika Philadelphia, Pennsylvania, nikiunganika na kundi namna ile ile, lenye tukio lile lile. Sina budi kuwa hivyo niwe Mkristo. Yanibidi nijiunganishe ambapo Neno la Mungu tayari linadhibitishwa.

159 Nimeunganika na kundi linalosikia Roho wa Mungu. Nimeunganika na kundi linalojua ya kwamba Yeye amefunuliwa linalojua ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na linajua ya kwamba huu si ushupavu wa dini, ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Mimi nimeunganika na kundi hilo

hapa usiku wa leo, hata ingawa wanaitwa kundi la wazushi, bado kundi la washupavu wa dini kwa ajili ya Neno la Mungu. Bali siionei haya Injili ya Yesu Kristo, kwa maana ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwao hao.

160 Niko pamoja nao, barua zilizo hai ambazo nilinena habari zake, zilizothibitishwa, Mungu aliyetiwa utaji katika umbo la mwanadamu ndani ya wanamume na wanawake. Lo Mungu katika *en morphe* Yake tena amejifunua na kujijulisha kwa watu Wake, mfalme mkuu aliyeweka kando utukufu Wake. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Nitafichwa kwao, bali ninyi mtaniona Mimi, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu kote kote hata utimilifu wote. Akibadilika kutoka Luther hata Wesley, na kadhalika, kutoka utukufu hata utukufu, Mimi ningali Mungu yule yule— ambaye anarudi kwenye ule utukufu wa asili." Haleluya!

161 Yeye amevunja kila utaji wa kidhehebu, kila kizuizi cha sauti. Hiyo sauti iliyosema, "Lo, huo ni ushupavu wa dini," ameivunjilia hiyo mbali.

162 Sauti iliyotoka humo na kusema, "Lo, watu hao wana kichaa," alivunjilia mbali utaji huo. Naam, Yeye alifanya hivyo.

163 "Lo, hamwezi kufanya hivyo. Ninyi si kitu ila kundi la washupavu wa dini!" Alivunja huo kabisa.

164 "Hamna kitu kama uponyaji wa kiungu." Yeye alivunja huo moja kwa moja (Jamani!), kwa maana Neno Lake lilisema angefanya hivyo. Hauwezi kushinda Neno la Mungu.

165 Na hapo yu asimama bado usiku wa leo, Mshindi aliye mkuu, tangu avunjulie mbali kila Methodisti, Batisti, Presbeteria, kila namna nyingine ya utaji. Yuangali anasimama mbele ya watu Wake usiku wa leo, hajashindwa na mapokeo. Na watu wasema wanavyotaka kusema, wanavyotaka, cho chote wanachotaka; Mungu yuaja moja kwa moja akivunjilia mbali kizuizi hicho cha sauti.

166 Na kumbukeni, wao huniambia ya kwamba eropleni inapovunja kizuizi hicho cha sauti hamna kikomo cha mbio zake. Nami nakwambia, unapovunjilia mbali hicho kizuizi cha mapokeo, ya kwamba "Yesu alikuwa kule nyuma kabisa na Yeye hayuko sasa," unapotambua ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hamna kikomo cha yale Mungu awezayo kutenda papa hapa katika mkutano huu, na kuonyesha ulimwengu huu wanachohitaji; si Maonyesho ya Ulimwengu, bali ufufuo wa ulimwengu utakaojazwa na kubatizwa kwa Uwepo wa Mungu Aliye Hai: *en morphe* akijifunika katika mwili wa kibinadamu. Haleluya.

167 Naamini kila kizuizi, kila utaji umevunjwa. Kila utaji, hamna kinachoweza kuuficha Uwepo Wake. Watu wanapopata njaa mioyoni mwao, kuna utaji ulio tayari kuvunjwa; unaweza tu kutumainia hilo. Kupasua kila utaji kwa Roho Wake aliye

mkuu. Naye yuasimama hapa usiku wa leo, Mshindi aliye mkuu; yeye yule jana, leo na hata milele; akiponya wagojwa; akiwabatiza waumini, jinsi alivyofanya. Yeye ni Mshindi aliye mkuu. Mashetani waliowekawa hukumu ya kifo wanakimbia. Naam, bwana! Wao hufanya hivyo kila wakati Yeye akiwepo.

168 Kwa kufunga, huenda nikasema hivi. Kulikuwa na . . . Nilisoma hadithi miaka mingi iliyopita kuhusu mzee mmoja mcheza fidla. Naye alikuwa na fidla kuu—kuu, naye alikuwa akitaka kuiuza. (Mmesikia hadithi hiyo mara nyingi:) Nao walitaka kuiuza kwa kiasi fulani. Mnadi akasema "Nani atakayenipa kiasi *fulani?"* Nami naamini ya kwamba alipewa sarafu chache, labda sumuni ama cho chote kile. "Mara ya kwanza, mara ya pili . . . "

169 Mara, mtu fulani akainuka huku nyuma; akasema, "Hebu kidogo," Yeye akaondoka akaenda na kuichukua. Hebu tuwaze kwamba alicheza huu:

Damu imebubujika
Ni ya Imanweli,
Wakioga wenye taka
Husafiwa kweli.

170 Basi, alipoiweka chini, hapakuwepo jicho kavu mahali hapo. Ndipo akasema, "Ni nani atakayetoa . . . "

Mmoja akasema, "Elfu tano."

"Elfu kumi."

171 Haingalinunulika kwa fedha. Kwani? M—mzee mtaalamu wa fidla alikwisha kuonyesha ubora wake halisi. Jamani, ndugu, dada, sasa, hebu na Mtaalimu wa Neno hili aliyeliandika, Roho Mtakatifu aliye mkuu, aupake uta wake utomvu wa pendo na kuuvuta kupitia moyoni mwako.

Damu imebubujika
Ni ya Imanueli . . .

172 Utaona dhamani yake dhahiri na umwone Mungu aliyefunuliwa akionekana wazi, ya kwamba ni yeye yule tu kama alivyokuwa aliposhuka katika siku ya Pentekoste juu ya watu, alipoji-*kenos* Mwenyewe, akajimiminia kwao. Hiyo ni kweli.

173 Unasema, "Ndugu Branham, nimejaribu nimejaribu. Nimefanya *hivi, vile* na *vinginevyo*."

174 Siku moja nilikuwa na mkutano huko Carlsbad, New Mexico; nasi tukaingia kwenye lile pango kubwa la popo kule chini; na ilionekana kijini. Nasi tukaingia mle; na—na mtu huyo alipoingia chini kule mahali hapa, a—akazima taa. Jamani, unaweza kuwaza jinsi ilivyokuwa giza! Ilikuwa—ilikuwa giza hivi kwamba ungeipapasa. Na hiyo ndiyo hali nyakati hizi ziko karibu kuwa. Tunapoona kanisa ambalo hushindwa kutambua Neno la Mungu; uonapa binti zetu wa Zayuni wakitenda

wanavyotenda; uonapa ndugu zetu ambao huvuta sigara, na kunywa pombe, na—na kufanya mizaha na kadhalika na huku wangali wanajaribu kushikilia maungamo yao katika Kristo (Jamani!); imekuwa giza; ni giza nene.

175 Tunaona ishara za kuja Kwake. Kutakuweko. . .Kila mara huwa giza sana kabla tu ya mapambazuko. Ndipo ile Nyota ya Asubuhi inachomoza kuiamkua siku, na kuitangulia na kuonyesha ya kwamba inakuja.

176 Tazama! Mle ndani, walipozima hiyo, kulikuweko msichana mdogo aliyelia kwa nguvu sana. Na kulikuweko mvulana mdogo aliyesimama karibu na yule kiongozi. Naye alimwona huyo kiongozi alipozima hizo taa, hivyo. Naye huyo dada mdogo nusura augue kwa ghafula. Alikuwa akipiga mayowe na kurukaruka juu chini, "Jamani, itakuweaje tena? Imekuwaje? Kuna nini?"

177 Unajua alivyomwambia kwa sauti kuu? Yeye alisema, "Usiogope, maskini Dadangu. Kuna mtu hapa ambaye anaweza kuwasha taa."

178 Sikiza, maskini Dadangu, huenda ukafikiri sisi ni wadogo na tu wachache sana, bali usiogope. Kuna Mtu hapa awezaye kuiwasha taa; huyo ni Roho Mtakatifu. Je, mnamwamini?

179 Hebu tuinamisheni vichwa vyetu kwa muda mfupi tu. Nasikitika nimekawisha sana. Ee Mungu mkuu wa Mbinguni, unayejifunua, ukijionyesha wazi, ukijifanya ujulikane Mungu mkuu wa Utukufu, chukua mafafanusi haya usiku wa leo na hebu yaiangukie mioyo ya watu. Nasi na tumwone Huyo aliyefunuliwa, ambaye alishuka na kupasua lile pazia la hekalu, ndiposa, akatoka moja kwa moja kwenye hilo pazia, akaja moja kwa moja akaingia katika pazia za wanadamu tena katika siku ya Pentekoste, amekuwa yule yule daima, akibadilika kutoka utukufu hata utukufu.

180 Sasa basi, tumerudi moja kwa moja kama maumbile yanavyotenda, moja kwa moja kurudia ile mbegu asili, moja kwa moja kutoka wakati mmoja wa kanisa hadi mwingine. Na wakati huu wa mwisho hapa, sisi hapa moja kwa moja kurudia kile kitu kilichoanguka kwenye siku ya Pentekoste kutimiza kila Andiko, Nuru katika wakati wa jioni, na "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya," Mambo mengi sana uliyoahidi katika Neno Lako.

181 Baba iwapo kuna mmoja hapa ambaye bado hajapasua hilo pazia, ama ikiwa kuna mmoja hapa ambaye amemwigiza tu mtu mwingine ambaye amekwisha kupita hilo pazia, toa neema usiku wa leo, Baba. Hebu na wamwone huyo Mshindi mkuu akisimama hapa, aliyejaa neema na uweza wa kusamehe. Tujalie, Bwana.

182 Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kungekuweko wengine humu. . .? Wangapi (naweza kusema hivyo) wangesema, "Ndugu Branham, nauinua mkono wangu. Niombee?" Endeleeni

kuinamisha vichwa vyenu na kuinua mikono yenu. “Nataka kuvunja nipite kila pazia miwezayo hata niweze kumwona yule Mshindi.” Mungu akubariki. Jamani—mikono hiyo! Kule nyuma kwenye roshani upande wa kuume. Mungu awabariki. Roshani kule nyuma. Mungu awabariki. Iweni waaminifu kabisa. Upande wa kushoto, inueni mikono yenu, mkasema, “Ndugu Branham, huenda nimekuwa Mkristo kwa miaka mingi, bali hakika, sijatoka kwenye hilo pazia. Sijafanya hivyo hakika. Sina hicho, walichokuwa nacho hapo awali.”

183 Leo tunacho, “Mimi ni mmea uliokuzwa katika tuta.” Chukua ua lililokuzwa katika tuta, huna budi kulitunza kama mtoto, kulibebeleza, kulinyunyizia dawa, kulinyunyizia maji; bali hilo ua la asili linalokua mle jangwani, ua la aina ile ile, linafanana nalo; halipati maji hata kidogo, bali hamna mdudu anayelifikia. Si laini. Ni halisi . . .

184 Ungelilinganisha Ukristo na, Ukristo wa siku hizi, na ulivyokuwa wakati huo? Ungewaza kundi hili, tunaloliita Wakristo siku hizi ulimwenguni kote, likiwa kama wao walivyokuwa baada ya Pentekoste, wakibebelezwa, na kupapaswa, na kutoka kanisa moja hadi lingine, na kusemwe jambo usilopenda na unainuka na kuondoka? Jamani! Ungewazia hilo? La! Kuna nini? Ni mwigizo.

185 Michelangelo, aliyeunda ile sanamu ya ukumbusho ya Musa . . . Unaweza kupata mwigizo wa hiyo kwa bei nafuu sana, bali ile ya asili . . . Yule aliyechora Meza ya Bwana . . . Nakisia hiyo picha asili ingegharimu dola milioni kadha, kama hata ungaliweza kuinunua. Sijui hata iliko. Bali unaweza kununua mwigizo wake kwa bei rahisi ya dola moja na senti tisini na nane. Unaweza.

186 Na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Mkristo rahisi, mwigizo, anayejiunga tu na kanisa, unaweza ukawanunua kwa sigara moja, ama—ama kinywaji cha kawaida. Au mwanamke aliyekata nywele zake, amepaka mdomo wake rangi, unaweza kumnunua kwa cho chote katika mitindo ya ulimwengu, bali hauwezi ukagusa yule aliye halisi.

187 Namwona Yeye akionekana dhahiri, yeye yule jana, leo, na hata milele. Jamani Wakristo, je, hamtaki kuwa Wakristo halisi? Iwapo kuna ye yote ambaye hakuinua mkono wake je unaweza kufanya hivyo tu niendapo kuomba. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Lo, hivyo ni sawa. Tazama tu . . .

188 Baba yetu uliye mbinguni, Neno Lako halitakurudia bure. Ni wewe uliyefanya ahadi. Wajibu wangu ni kusema tu ya kwamba Wewe ulisema hivyo. Ninarudia tu maneno Yako. Ulisema, “Yeye asikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa milele.” Wewe uliahidi. Na, Bwana, tunajua tunayo hiyo miigizo siku hizi, wengi ambao wanasema wao wanaamini

bali hawaamini; wanaonekana. Bali, Bwana, kuna walio wa kweli pia.

189 Naomba ya kwamba utatujalia hapa usiku wa leo ya kwamba kila mwanamume na mwanamke, mvulana au msichana, haidhuru wako katika taifa gani, niwa rangi gani, ni wafuasi wa kanisa gani . . . Ee, Mungu, wajaze. Hebu na waone dhihirisho halisi la Yesu yuyo huyo akiwemo miongoni mwetu, kama alivyokuwa siku ya Pentekoste alipojifunua Mwenyewe kwa ajili ya kizazi hiki, akiwa Roho Mtakatifu. Tujalie.

190 Tunapoona Neno limetimizwa, unabii umetimia, tunalinganisha siku hizi kile kinachoitwa kanisa la ulimwengu—au Baraza la Makanisa Ulimwenguni, na kulilinganisha hayo na ile ahadi katika Pentekoste; hakuna ulinganifu kamwe. Hatuwezi kufuliwa nguo zetu chafu na tiketi hiyo.

191 Bali, Bwana Mungu, iwapo tutarudi kwenye hiyo chemichemi, mna njia ya kusafishia. Ndipo ujuzi wetu na Neno la Mungu vitalingana zote mbili; basi tunaweza kudai mali yetu. Tujalie, Bwana, usiku wa leo, ninapowakabidhi watu hawa mikononi Mwako. Mpe kila mmoja mahitaji yetu, baba. Twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

192 Mungu awabariki. Asanteni sana kwa kusimama, kungoja kwa muda mrefu, nami nasikitika naliwakawisha hata saa nne na dakika kumi. Mungu awe nanyi hata nitakapowaona asubuhi. Nairudisha ibada hii sasa, nakisia, kwa msimamizi sherehe.

Mungu Aliye Mkuu Akifunuliwa Mbele Zetu SWA64-0629
(The Mighty God Unveiled Before Us)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatatu jioni, Julai 29, 1964, kule Philadelphia, Pennsylvania, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2014 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org